/ISSN 0856 - 034X

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

***Supplement No. 5*** ***11th September, 2023***

## *SPECIAL SUPPLEMENT*

*To The Gazette of the United Republic of Tanzania No. 25 Vol. 104 Dated 11th September, 2023*
Printed by The Government Printer, Dodoma by Order of Government

TANGAZO LA SERIKALI NA. 664A la terehe 11/9/2023

KATIBA YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA YA MWAKA 1977,
(SURA YA 2)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya Ibara ya 89 ya Katiba na kanuni ya 176(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023)*

KANUNI ZA MAREKEBISHO YA NYONGEZA YA NANE YA KANUNI ZA KUDUMU ZA BUNGE ZA MWAKA 2023

Jina

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Marekebisho ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2023 na zitasomwa pamoja na Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, ambazo katika Kanuni hizi zinarejewa kama "Kanuni kuu".

Marekebisho ya Nyongeza ya Nane

2. Kanuni kuu zinarekebishwa kwa kufuta Nyongeza ya Nane na badala yake kuweka Nyongeza ya Nane mpya ifuatayo:

"___________

# NYONGEZA YA NANE

# KAMATI ZA KUDUMU ZA BUNGE

*(Chini ya Kanuni ya 137)*

## SEHEMU YA KWANZA
## KAMATI ZA KUDUMU ZISIZO ZA SEKTA

Kamati za Kudumu zisizo za kisekta

1. Kamati za Kudumu zisizo za Kisekta zitakuwa zifuatazo:
   (a) Kamati ya Uongozi;
   (b) Kamati ya Kanuni za Bunge; na
   (c) Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge.

Muundo na majukumu ya Kamati ya Uongozi

2.-(1) Kamati ya Uongozi itakuwa na Wajumbe wafuatao:
   (a) Spika, ambaye atakuwa Mwenyekiti;
   (b) Naibu Spika, ambaye atakuwa Makamu Mwenyekiti;
   (c) Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni au Mwakilishi wake;
   (d) Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Walio Wachache Bungeni au Mwakilishi wake;
   (e) Mwanasheria Mkuu wa Serikali; na
   (f) Wenyeviti wa Kamati za Kudumu au Makamu wao.

(2) Katibu atakuwa Katibu wa Kamati.

(3) Majukumu ya Kamati ya Uongozi yatakuwa ni kujadili na kumshauri Spika kuhusu mambo yote yanayohusu uendeshaji bora wa Shughuli za Bunge, na utaratibu wa kurahisisha uendeshaji wa Shughuli za Bunge au za Kamati yoyote.

(4) Katika kutekeleza kazi zilizotajwa katika fasili

ya (3), Kamati ya Uongozi itakuwa na uwezo wa kuweka muda ambao shughuli yoyote iliyopelekwa katika Kamati inayohusika sharti ikamilike, na iwapo shughuli iliyopelekwa imewekewa muda kama huo, basi baada ya kuisha muda huo au baada ya kuisha muda wowote ulioongezwa, Kamati inayohusika itahesabiwa kuwa imemaliza shughuli hiyo, na shughuli hiyo itaendelea kwenye hatua nyingine kana kwamba Mwenyekiti wa Kamati hiyo amemuarifu Spika kumalizika kwa shughuli hiyo.

Muundo na Majukumu ya Kamati ya Kanuni za Bunge

3.-(1) Kamati ya Kanuni za Bunge itakuwa na Wajumbe wafuatao:

(a) Spika ambaye atakuwa Mwenyekiti;
(b) Naibu Spika ambaye atakuwa Makamu Mwenyekiti;
(c) Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Walio Wachache Bungeni au Mwakilishi wake;
(d) Wenyeviti wa Bunge;
(e) Mwanasheria Mkuu wa Serikali; na
(f) Wajumbe wengine watakaoteuliwa na Spika.

(2) Vikao vya Kamati ya Kanuni za Bunge vitaongozwa na Spika, na kama Spika hayupo, vitaongozwa na Naibu Spika.

(3) Majukumu ya Kamati ya Kanuni za Bunge yatakuwa ni-

(a) kujadili na kutoa mapendekezo juu ya kufanya marekebisho au mabadiliko katika Kanuni;
(b) kuchunguza na kutoa taarifa juu ya pendekezo lolote la mabadiliko katika Kanuni za Kudumu za Bunge ambalo limepelekwa kwa Kamati hiyo na Spika au na Mbunge yeyote;
(c) kuchunguza na kutoa taarifa kuhusu malalamiko dhidi ya Uamuzi wa Spika ambayo yamepelekwa kwenye Kamati hiyo na Spika;
(d) kwa kushauriana na Spika, kuzifanyia marekebisho au mabadiliko Nyongeza za Kanuni;

(e) kumshauri Spika kuhusu masuala ya ukiukwaji wa Kanuni au suala lolote linalohusu utaratibu; na

(f) kushughulikia malalamiko dhidi ya matokeo ya uchaguzi unaofanyika kwa mujibu wa Nyongeza ya Pili ya Kanuni hizi.

(4) Akidi ya kikao cha Kamati ya Kanuni za Bunge itakuwa ni nusu ya wajumbe waliotajwa katika aya ya 3(1)(c), (d), (e) na (f).

Majukumu ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge

4.-(1) Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge itatekeleza majukumu yafuatayo:

(a) kuchunguza na kutoa mapendekezo kuhusu masuala yote ya haki, kinga na madaraka ya Bunge yatakayopelekwa na Spika;

(b) kushughulikia mambo yanayohusu maadili ya Wabunge yatakayopelekwa na Spika; na

(c) kushughulikia shauri linalomhusu Mbunge anayewakilisha Bunge kwenye chombo kingine cha uwakilishi au Mjumbe wa Bunge la Afrika Mashariki.

(2) Kamati itakapokamilisha kushughulikia jambo husika, Mwenyekiti wa Kamati atamjulisha Spika kwa maandishi kwamba, Kamati imemaliza kujadili jambo husika.

(3) Spika baada ya kupokea taarifa hiyo, ataagiza iwekwe kwenye orodha ya Shughuli za Bunge kwa ajili ya kuwasilishwa na kujadiliwa Bungeni.

## SEHEMU YA PILI
## KAMATI ZA KUDUMU ZA BUNGE ZA KISEKTA

Kamati za Kudumu za kisekta

5. Kamati za Kudumu za Bunge za Kisekta zitakuwa zifuatazo:

(a) Kamati ya Viwanda, Biashara, Kilimo, Mifugo;

(b) Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria;

(c) Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama;

(d) Kamati ya Tawala za Mikoa na Serikali za

Mitaa;
(e) Kamati ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii;
(f) Kamati ya Maji na Mazingira;
(g) Kamati ya Elimu, Utamaduni na Michezo;
(h) Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii;
(i) Kamati ya Afya na Masuala ya UKIMWI;
(j) Kamatiya Miundombinu; na
(k) Kamati ya Nishati na Madini.

Kamati na shughuli za Wizara

6.-(1) Kamati ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo itasimamia Wizara zifuatazo:
(a) Wizara ya Viwanda na Biashara;
(b) Wizara ya Kilimo; na
(c) Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

(2) Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria itasimamia shughuli za Wizara zifuatazo:
(a) Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora;
(b) Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji;
(c) Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira katika masuala ya Muungano;
(d) Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Uratibu na Bunge; na
(e) Wizara ya Katiba na Sheria.

(3) Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama itasimamia shughuli za Wizara zifuatazo:
(a) Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki;
(b) Wizara yaUlinzi na Jeshi la Kujenga Taifa; na
(c) Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

(4) Kamati ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa itasimamia shughuli za Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

(5) Kamati ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii itasimamia shughuli za Wizara zifuatazo:

(a) Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Ajira na Wenye Ulemavu; na

(b) Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum.

(6) Kamati ya Maji na Mazingira itasimamia shughuli za:

(a) Wizara ya Maji; na

(b) Masuala ya Mazingira katika Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira.

(7) Kamati ya Elimu, Utamaduni na Michezo itasimamia shughuli za Wizara zifuatazo:

(a) Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia; na

(b) Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo.

(8) Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii itasimamia shughuli za Wizara zifuatazo:

(a) Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; na

(b) Wizara ya Maliasili na Utalii.

(9) Kamati ya Afya na Masuala ya UKIMWI itasimamia shughuli za:

(a) Wizara ya Afya; na

(b) Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania.

(10) Kamati ya Miundombinu itasimamia shughuli za Wizara zifuatazo:

(a) Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi; na

(b) Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

(11) Kamati ya Nishati na Madini itasimamia shughuli za Wizara zifuatazo:

(a) Wizara ya Nishati; na

(b) Wizara ya Madini.

Majukumu ya jumla ya Kamati za Sekta

7.-(1) Majukumu ya Kamati ya Kudumu ya Bunge za Sekta yatakuwa yafuatayo:

(a) kushughulikia bajeti ya Wizara inazozisimamia;

(b) kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia;

(c) kushughulikia Taarifa za utendaji za kila

mwaka za Wizara hizo; na

(d) kufuatilia utekelezaji unaofanywa na Wizara hizo.

(2) Bila kuathiri majukumu ya jumla ya Kamati za kisekta kama yalivyoainishwa katika fasili ya (1) Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama itatekeleza pia majukumu yafuatayo:

(a) kuimarisha ushirikiano kati ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mabunge ya nchi nyingine;

(b) kufuatilia mwenendo na hali ya mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika;

(c) kushughulikia taarifa za wawakilishi wa Tanzania katika Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika na Bunge la Afrika;

(d) kushughulikia Taarifa zote za wawakilishi katika Vyama mbalimbali vya kibunge ambapo Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mwanachama; na

(e) kushughulikia taarifa za hali ya ulinzi na usalama wa mipaka ya nchi na usalama wa raia na mali zao.

## SEHEMU YA TATU
## KAMATI ZA SEKTA MTAMBUKA

Kamati za Sekta Mtambuka

8. Kamati za Sekta Mtambuka zitakuwa zifuatazo:

(a) Kamati ya Bajeti;

(b) Kamati ya Sheria Ndogo; na

(c) Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma.

Majukumu ya Kamati ya Bajeti

9. Isipokuwa kama imeelekezwa vinginevyo katika Kanuni hizi, Kamati ya Bajeti itatekeleza majukumu yafuatayo:

(a) kusimamia shughuli za Wizara ya Fedha;

(b) kusimamia shughuli za Tume ya Taifa ya

Mipango;

(c) kujadili na kutoa maoni na ushauri kuhusu uandaaji wa mwongozo wa kutayarisha Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa kila mwaka;

(d) kutathmini na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali ya kila mwaka yatokanayo na vyanzo vya kodi na vyanzo vingine visivyo vya kodi;

(e) kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali;

(f) kuchambua na kushauri kuhusu Miswada ya Sheria inayowasilishwa Bungeni yenye madhumuni ya kuongeza au kupunguza mapato na Bajeti ya Serikali;

(g) kufanya utafiti na uchambuzi kuhusu sera za kodi, sera za fedha, na sera za kiuhasibu zilizopendekezwa na Serikali;

(h) kujadili na kutoa maoni na ushauri kuhusu vyanzo vya mapato ya Serikali na mapendekezo ya hatua za kupunguza utegemezi wa kibajeti;

(i) kutoa ushauri wa jumla kuhusu Bajeti ya Serikali kwa Bunge na Kamati za Kudumu za Bunge;

(j) kuchambua na kutoa maoni na ushauri kuhusu Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaopendekezwa na Serikali; na

(k) kuchambua hoja zitakazojitokeza kwenye Kamati za Bunge za Kisekta wakati wa kujadili Bajeti za Wizara kwa ajili ya kuishauri Serikali.

Majukumu ya Kamati ya Sheria Ndogo

10.-(1) Kamati ya Sheria Ndogo itakuwa na majukumu ya kuchambua Sheria Ndogo ili kujiridhisha iwapo zimekidhi matakwa na masharti ya Katiba, sheria inayotekelezwa na sheria ndogo husika pamoja na sheria nyingine za nchi.

(2) Kamati itakapokamilisha kazi kwa mujibu wa fasili ya (1), Mwenyekiti atamjulisha Spika kwa maandishi.

(3) Spika, baada ya kupokea taarifa chini ya fasili ya (2), anaweza kuelekeza Taarifa ya Uchambuzi wa Kamati iwekwe kwenye orodha ya Shughuli za Bunge kwa ajili ya kuwasilishwa na kujadiliwa Bungeni.

Majukumu ya Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma

11.-(1) Majukumu ya Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma yatakuwa kama ifuatavyo:

(a) kuchambua na kubaini iwapo utekelezaji wa miradi ya uwekezaji wa umma una ufanisi na kuwa umezingatia taratibu na sheria na miongozo mujarabu ya biashara; na

(b) kuchambua na kujadili taarifa zinazohusu uwekezaji katika mashirika ya umma na kampuni ambazo Serikali ina hisa.

(2) Msingi wa kazi za Kamati utatokana na taarifa zinazohusu uwekezaji katika mashirika ya umma na kampuni ambazo Serikali ina hisa.

## SEHEMU YA NNE
## KAMATI ZA KUDUMU ZA BUNGE ZINAZOSIMAMIA MATUMIZI YA FEDHA ZA UMMA

Kamati za Kudumu za Bunge zinazosimamia matumizi ya fedha za umma

12. Kamati za Kudumu za Bunge zinazosimamia matumizi ya fedha za umma zitakuwa zifuatazo:

(a) Kamati ya Hesabu za Serikali; na

(b) Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa.

Majukumu ya Kamati ya Hesabu za Serikali

13. Majukumu ya Kamati za Hesabu za Serikali yatakuwa yafuatayo:

(a) kushughulikia maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha za umma katika Wizara za Serikali na mashirika ya umma yaliyoainishwa katika Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali;

(b) kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yaliyokwishatolewa na Kamati ili kuondoa matatizo yaliyobainika kwa mujibu wa kanuni hii; na

(c) kutoa mapendekezo na ushauri kwa Wizara za Serikali na Mashirika ya Umma kuhusu matumizi mazuri ya fedha za Umma ili kupunguza matumizi mabaya ya fedha za Umma.

Majukumu ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa

14. Majukumu ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa yatakuwa kama ifuatavyo:

(a) kushughulikia maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha za Serikali za Mitaa yaliyoainishwa katika Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali;

(b) kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yaliyokwishatolewa na Kamati ili kuondoa matatizo hayo; na

(c) kutoa mapendekezo na ushauri kwa Serikali za Mitaa kuhusu matumizi mazuri ya fedha ili kuhakikisha kwamba, tatizo la matumizi mabaya ya fedha za Umma linapungua.

Msingi wa kazi za Kamati ya Hesabu za Serikali na Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa

15. Msingi wa kazi za Kamati ya Hesabu za Serikali na Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa utatokana na Taarifa za Hesabu zilizokaguliwa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.”.

Dodoma,
4 Septemba, 2023

TULIA ACKSON
*Spika wa Bunge*